

Pambazuko

Toleo Namba 0048

Jumatatu Septemba 25-Oktoba 1, 2023



**Wawekezaji
Soko la Hisa
wakimbia**

Uk. 7

Soko la dawa Tanzania ni salama

- WHO yathibitisha, TMDA yakaza kamba
- Nchi jirani zaja kujifunza mbinu, utaalamu

Uk. 4

**Kampuni
za bima
zaondoa
woga**

Uk. 10

JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

Tahariri

Labda, tuwe na wizara ya umeme tu

KUKOSEKANA kwa nishati ya umeme - mara kwa mara katika maeneo mengi nchini, ni moja ya sababu za kuwepo ongezeko la ufukara kwa Watanzania.

Ushahidi kwamba kutokuwepo nishati hiyo kunaongeza ufukara kwa wananchi, huonekana dhahiri kwa kusimama kwa shughuli nyingi za uzalishaji ambazo hutegemea nguvu ya umeme.

Endapo hakuna umeme, viwanda husimama; vituo vidogo na vikubwa vya kuzalisha mali husindwa kuendelea; wajasirimali wa kuuza mahitaji mbalimbali hufunga shughuli zao na wenye migahawa hulazimika kusimama kutoa huduma kwa kuwa hakuna nishati hiyo muhimu.

Hata hivyo, pamoja na ukweli huo, bado nchi yetu, kupitia serikali inayosimamia maendeleo, inakwamba kuhakikisha kunakuwepo umeme wa uhakika.

Miaka nenda-rudi, serikali imekwama kukomesha tatizo la kukosena kwa umeme, licha ya kuwepo ahadi lukuki kutoka kwa kila rais anayeingia madarakani.

Na siyo kiongozi wa nchi tu, hata mawaziri wakuu na mawaziri wa nishati waliowahi kuwepo katika wizara, wako katika rekodi wakitoa kutoa ahadi kwamba “mgawo wa umeme, utakuwa historia.”

Hata hivyo, viongozi wote hao, hakuna ambaye ahadi yake ilitimia kwa asilimia hata 60 ya uhakika wa kuwepo umeme mpaka wanaondoka kwenye dhamana.

Malalamiko ya wananchi yamekuwa ni “kawaida” kuhusu kukatika mara kwa mara kwa umeme na kukwamisha shughuli zao za maendeleo, hivyo kuzidisha ufukara

na madhila mengine ya maisha yanayotokana na shida ya nishati inayorahisisha shughuli zao za kuleta kipato.

Sababu zinazoletwa na viongozi wetu kuhusu kukatika kwa umeme, nyingine zinaeleweka, lakini nyingi hazieleweki, kutokana na kushindwa kubeba ukweli wa hali halisi.

Wapo viongozi waliotuaaminisha kwamba kusimikwa kwa mitambo ya majenereta ya kufua umeme kwa mafuta mazito ndiyo mwarobaini wa kadhia hiyo, lakini ilipofungwa – kwa hatua za dharura na haraka na kuanza kazi, haikuwa dawa. Mgawo ulibaki palepale.

Tukaeleza pia kwamba dawa ya kuondokana na tatizo la umeme ni kuongeza mabwawa ya kuzalisha umeme, ikafanyika hivyo, lakini hakuna kilichotibika, mgawo ukaendelea.

Viongozi wengine wa nchi yetu wakaona shida siyo mitambo wala maji, ni mawaziri; basi mawaziri wakadilishwa kila uchao, lakini bado tatizo liko palepale.

Sisi katika Pambazuko, tunadhani, wizara ya nishati ni “dubwashika” kubwa hivi ambalo limebeba vitu vingi, na wahusika, hasa mawaziri wake wanashindwa kulimudu, kwa kukosa muda mzuri wa “kudeal” na umeme tu.

Hivyo basi, tunaamini ipo haja ya kuwepo Wizara ya Umeme pekee, ambayo itakuwa mahsusi kushughulikia nishati hiyo pekee.

Tukiwa na wizara yenye kuhusika na umeme pekee, huenda mawaziri na wasaidizi wao wakabeba ubunifu wa kutuondoa kwenye shida hii kubwa ya kukatika – mara kwa mara kwa nishati hiyo.

CHAI ISINICHELEWESHE...



Rais wa Kenya, William Ruto akiwahi kikao baada ya kuchukua kikombe cha chai. Hii ilikuwa mapema mwezi huu jijini Nairobi, ambako kulikuwa na mkutano mkubwa wa viongozi wa Afrika uliofanyika kujadili mabadiliko ya tabia nchi. (Picha na Ikulu ya Kenya).

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko1@protonmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

NUKUU



Mwanaume ukifikia miaka zaidi ya hamsini, tambua na kubali kwamba umri umeenda, kwanini kuhangaika na dawa za kuongeza nguvu za kiume? Unaweza kabisa kuibua magonjwa mengine makubwa zaidi. Hakuna ujanja, kubali tu ukweli wa uzee - Dkt. Danstan Shewiyo; Mkurugenzi wa Maabara, TMDA.

Habari**Soko la dawa Tanzania ni salama**

Na Mwandishi WETU

WATUMIAJI na wasambazaji wa dawa anuai; za binadamu na mifugo katika soko la Tanzania, hawana sababu ya kuwa na hofu ya ubora wa bidhaa hiyo kwa kuwa ni salama, Pambazuko linabainisha.

Shukurani za pekee zinaelekezwa kwa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba ya Tanzania (TMDA) kwa umakini katika kuzuia, kudhibiti, kung'amua na kuchukua hatua za haraka kwa dawa feki, zisizokuwa na ubora na hata zilizopitwa muda wa matumizi.

Ubora na umahiri wa maabara za TMMDA unathibitishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) katika taarifa zake za hivi karibuni; miaka miwili mfululizo.

Akizungumza na Pambazuko, Mkurugenzi Mkuu wa TMMDA, Adam Fimbo anaeleza kwamba maabara ya mamlaka anayoiongoza imepewa ithibati na WHO na taasisi zingine za kimataifa kwa ubora wake na umahiri katika kupima na kung'amua kila chembe ya "kiungo" cha dawa zote zinazolingia ama kutengenezwa Tanzania.

Fimbo anasifu uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa umakini katika kujali afya za wananchi anaowaongoza, kwani serikali imewekeza kiasi kikubwa cha fedha kununua vifaa na vitendanishi kwa ajili ya kufanya kazi kwa ufanisi.

Kutokana na ufanisi wa kazi zake za kufuatilia usalama wa dawa, vifaa tiba, vitendanishi na bidhaa za afya, TMMDA ina rekodi ya kuwa kituo cha umahiri unaotambuliwa na (WHO) na Kituo cha Umahiri wa Usajili wa Dawa Afrika.

"Mwaka 2017 tulifanikiwa kuanzisha mazingira wezeshi na rafiki ya kufanya biashara nchini kwa bidhaa zinazodhibitiwa na TMMDA, 2018 tukafikia ngazi ya tatu ya WHO (WHO Maturity L-3) kwa kuwa na mifumo bora ya udhibiti dawa Afrika," ameongeza bingwa huyo



Adam Fimbo - Mkurugenzi Mkuu TMMDA

wa kuchunguza na kuthibiti ubora wa dawa.

Mkurugenzi wa Huduma za Maabara wa TMMDA, Dkt. Danstan Shewiyo ameliambia Pambazuko kwamba maabara ya mamlaka yake ni bora zaidi katika Afrika na imekuwa ikitumiwa na nchi kadhaa kufuatilia na kudhibiti dawa zinazolingia nchini mwao.

Anazitaja nchi ambazo zimekuwa zikileta dawa kupimwa ubora nchini Tanzania kuwa ni pamoja na Lesotho, Burundi, Zambia, Msumbiji na Liberia.

"Nchi nyingi zinaleta dawa hapa kufanyiwa utafiti kabla ya kuruhusiwa kwenye masoko ya nchi hizo, na karibuni tulihusika kuzuia dawa tulizobaini zina madhara kwa binadamu katika nchi ya Gambia na ilikuwa ni hatua nzuri iliyoooka maisha ya watu," anaongeza daktari huyo.

Dkt. Shewiyo anasema taarifa za WHO, kwa miaka miwili mfululizo, inatangaza maabara ya udhibiti wa Tanzania kuwa katika hatua ya nne ya viwango vya ubora, sawa na nchi za Marekani, Uingereza na Canada.

Kagera Sugar, ondoeni vumbi Bunazi

Na Igo AI

BAADA ya kumalizana na Ikulu, Tai alipigiwa simu na wadau wake walioko Wilaya ya Missenyi, Kagera - tena hawa wanatoka eneo la Bunazi.

Hawa ni wakaazi wa pembezoni mwa Barabara ya Kagera Sugar, ambayo inaanzia hapo Bunazi. Wapo wanaoishi nyumba zinazotazama barabara hiyo na wapo wanaofanya biashara zao hapo.

Barabara hiyo ni maarufu na ndiyo iko "bize" mno kwa kuwa inapitisha magari makubwa yakiwa yamesheheni miwa kutoka mashambani kupeleka kiwandani.

Huko kiwandani ndiko kunazalishwa sukari ambayo ni muhimu mno katika kukamilisha vyakula mbalimbali kwa matumizi ya binadamu.

Hata hivyo, wakazi hao hawana shida na utamu unaozalishwa na kiwanda hicho, kwa maana ya sukari, lakini ipo shida kubwa.

Wakazi wa eneo hilo wanalalamikia kuwepo kwa vumbi jingi linalotimka wakati magari hayo makuukuu yanayobeba marundo ya miwa yanapopita kwenda kiwandani ama yanapotoka bila mzigo.

Barabara haina lami, wala haina moramu, wala kokoto, sasa ni vumbi mtindo mmoja.

Wakazi hao wamemweleza tai shida na kero yao hiyo. Tai akaona isiwe taabu, na hapendi kuelezwa uongo. Lazima aende akathibitisha.

Basi, tai akapanga safari, akaruka hadi mpakani mwa Tanzania na Uganda, pale eneo la Mutukula, akafika salama, akatafuta mahali ili ale matoke na maharagwe meupe.

Baada ya kujishibia zake, akaruka hadi Bunazi. Akatua juu ya paa la jengo moja hapo Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi.

Akang'ang'aza jicho lake moja na kukutana na vumbi lisilokuwa la kawaida, likirushwa na magari yanayopita kwenye barabara jirani, hivyo haraka haraka akagundua ndiyo barabara anayoisaka.



Miwa

Basi bwana, akajipa moyo kwanza asogee zaidi ili apate picha na ushahidi wa hicho alichoelezwa na wadau wake.

Mhhh! Kwani alikaa tena, alikabwa na chafya nyingi za hatari. Vumbi likamzonga kooni na machoni, hakuona tena hata magari yaliyokuwa yakipita; ni vumbi tu limemjaa kila mahali. Kichwa kikageuka kuwa rangi ya udongo, kope zimezibwa kwa vumbi na chafya ndiyo usiseme.

Akaamua kujiondokea na kurejea makazi yake Dar es Salaam, ili aandike taarifa hii.

Hakika watu wa Bunazi wanateseka kwa vumbi na kweli wamelalamika, lakini siyo Kiwanda cha Sukari cha Kagera, wala halmashauri wanaowajibika kuzuia ama kupunguza vumbi hilo.

Wajameni, hebu Kagera Sugar, ama Halmashauri ya Missenyi na uongozi wa Mkoa wa Kagera, wasikilizeni watu wa Bunazi. Vumbi linawaua hata kama hawasemi!

Hivi nini kinashindikana kuweka lami, ama moramu kwenye barabara hiyo ambayo inaelekea kwenye eneo la uwekezaji mkubwa wa uzalishaji wa sukari?

Ahh! Hebu epusheni magonjwa ya mfumo wa hewa, macho na mengine yanayosababishwa na vumbi jingi katika barabara hiyo.

Inawezekana. Kazi ifanyike kuokoa maisha ya watu wa Bunazi.

Habari

Wawekezaji Soko la Hisa wakimbia

Na Tryruckia MFINANGA

KASI ya wawekezaji wa kigeni kukimbia masoko ya hisa ya nchi zinazoendelea, ikiwamo Tanzania, imeongezeka, Pambazuko limebaini.

Wengi wa wawekezaji hao wamekuwa wakiuza hisa zao kwenye masoko hayo kwa bei ya punguzo kutokana na kudorora kwa thamani ya fedha za nchi husika.

Pambazuko limeelezwa pia kwamba sababu nyingine kubwa ya wawekezaji kuuza hisa zao ni ongezeko la riba za Benki Kuu kwenye nchi zenye uchumi mkubwa – wanakokimbizia mitaji yao kwenye masoko ya fedha kupitia hati funguni na amana za muda maalumu.

Marekani ni kati ya nchi ambazo zimeongeza riba kwenye masoko yake ya fedha, kwa zaidi ya miezi mitatu sasa, riba za Benki Kuu (Federal Reserve) imefikia kiwango cha juu cha asilimia tano na nusu (5.5%) na wachambuzi wanavyotabiri kwamba huenda riba ikapanda zaidi baadaye kutokana na mwenendo wa sera ya fedha ya nchi hiyo.

Baadhi ya wachumi na wapembuzi wa masoko ya hisa duniani wameliambia Pambazuko kwamba katika kipindi cha “kuadimika” kwa dola ya Marekani, kampuni zilizowekeza kwenye masoko ya hisa Marekani, ziliongeza gawio ili kuvutia wawekezaji, na kampuni hizo zilifanikiwa kukusanya kiasi kikubwa cha mitaji mipya kutoka nchi zinazoendelea ikiwamo Tanzania; hivyo kuongeza mzunguko wa fedha.

Ifahamike kuwa Soko la Marekani linatokana na mchanganyiko wa nguzo tatu, kila moja inawakilisha soko la hisa na imepewa jukumu la kusimamia sekta ya fedha ya Marekani na kampuni za kigeni. Nguzo hizo ni Soko la Hisa la New York (NYSE), Nasdaq na Soko la Hisa la Chicago (CHX).

Ripoti za Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) zinaonyesha kuwa katika kipindi



Mary Mniwasa- Kaimu Mtendaji Mkuu wa DSE

cha robo ya tatu ya mwaka huu inayoshia Septemba hii, wawekezaji hao wameuza hisa zenye thamani ya shilingi bilioni 13, nyingi zikiwa zile za kampuni kubwa zilizoorodheshwa kwenye soko hilo.

Katika kipindi hicho hicho, kinyume chake, wawekezaji hao wa kigeni wamenunua hisa zenye thamani ya shilingi milioni 805 tu, zinazotajwa kuwa ni kiwango cha chini kabisa kuwahi kutokea cha ununuzi katika historia ya soko hilo.

Ripoti hiyo imeonyesha pia kwamba katika kipindi cha kuanzia Aprili Mosi, hadi Septemba 21, wawekezaji wa kigeni wameuza hisa zao zenye thamani ya shilingi bilioni 31 kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam, huku wakinunua hisa zenye thamani ya shilingi bilioni 17 pekee, kati ya hizo shilingi bilioni 16 zikiwa zimenunuliwa kweye robo ya pili ya mwaka huu.

Hata hivyo, hisa zote zilizouzwa na wawekezaji wa kigeni, zilinunuliwa na wawekezaji wa ndani, hali inayoonyesha uhimilivu wa dhoruba za uwekezaji.

Madalali wa DSE wameliambia Pambazuko kwamba hali hii itaendelea katika kipindi kijacho, ambapo wawekezaji hao wanawekeza fedha zao

Inaendelea Uk. 7

Wawekezaji Soko la Hisa wakimbia

Inatoka Uk. 6

kwenye masoko ya dhamana ya nchi zilizoendelea, ikiwamo Marekani na nchi za Ulaya, ambako viwango vya riba vinaendelea kupanda.

Kadhalika, madalali hao wanasema kuwa sababu nyingine ya wawekezaji hao kukimbia ni uhaba wa fedha za kigeni, hasa dola ya Marekani, hali inayosababisha kushuka kwa thamani ya sarafu za ndani, ikiwamo sarafu ya Tanzania.

Ripoti za DSE zinaonyesha kwamba kiasi kikubwa cha mauzo kimetokana na uuzwaji wa hisa za kampuni kubwa ambazo ni Kampuni ya Bia Tanzania (TBL), Kampuni ya Sigara Tanzania (TCC), Benki za CRDB na NMB, na za kampuni ya simu za mkononi; Vodacom, ambazo zinauzwa kwa bei ya punguzo.

“Wawekezaji wa kigeni wataendelea kuwa na wasiwasi na masoko ya nchi zinazoendelea, ikiwamo Tanzania, hasa wale waliowekeza kwenye kampuni kubwa nchini,” anasema Raphael Masumbuko, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Zan Securities, madalali wa hisa wa DSE.

Masumbuko anasema kwamba kwa upande wa Tanzania, kumekuwa na mwendelezo wa wawekezaji wa kigeni kuondoka kwenye soko, hali iliyosababisha kuwa na nakisi kubwa ya kiwango cha mauzo ya hisa zao, dhidi ya hisa wanazonunua, na upungufu wa fedha za kigeni ikiwa ni moja ya sababu.

Imani Muhingo, mkuu wa kitengo cha utafiti na uchambuzi wa Alpha Capital, Dar es Salaam, anasema wawekezaji kuhamisha mitaji yao ni jambo ambalo limezikumba nchi nyingi zinazoendelea kutokana na hali ya sasa ya uchumi wa dunia.

Anasema hali hiyo imesababisha wawekezaji wengi kuhamia kwenye masoko ya nchi zilizoendelea ambako uwekezaji wao unapata faida nono kutokana na viwango vya riba na uimara



Dkt. Mwigulu Nchemba- Waziri wa Fedha

wa uchumi.

Watanzania washindwa kuchangamka Maana halisi ya hisa ni ununuzi wa umiliki wa sehemu ya kampuni ambayo inaruhusu sehemu yake ya faida kugawanywa kwa wahusika.

Faida inayopatikana hugawanywa kwa waliowekeza fedha zao na wakati mwingine mwekezaji huuza hisa zake kwa wengine.

Katika Tanzania, utamaduni wa kuwa na hisa kwenye kampuni bado hauna mwamko wa kutosha, kwani Soko la Hisa la Tanzania bado lina idadi kubwa ya wawekezaji wasiokuwa “wazawa.”

Uwekezaji huu umeendelea kuwanufaisha wageni zaidi kuliko Watanzania ambao ndio wanaostahili kushiriki katika uchumi wao.

Ileweke pia kwamba mbali ya kuuza hisa ama kupata gawio, mwekezaji anaweza kutumia hati ya hisa kama dhamana pale anapohitaji kukopa kwenye taasisi za fedha.

Hasara katika uwekezaji ipo endapo kutatokea kushuka kwa thamani ya hisa zako au kutokupatikana kwa gawio kwa mwekezaji kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo uchumi wa nchi husika kudorora.

Tangazo

Ukiwa Bukoba...

Furahia Nene Freshi Juisi

Pata juisi (sharubati) ya matunda halisi iliyoandaliwa kwa usafi wa hali ya juu kwa kujali afya ya mteja.

Kunywa juisi ya;

Embe	Nanasi/pinacolada
Passion	Tende
Parachichi	Tikiti
Karoti	

Pia tunandaa juisi mchanganyiko maalum wa matunda ili kuondoa uchovu na magonjwa nyemelezi (detox) na pia smoothie.

Waziliana nazi kwa
namba hii:

0753949488





Hoja Yangu

Tuibane G20 kuokoa mazingira Afrika

Na Rashid Mtagaluka

HATIMAYE mkutano unaowajumuisha viongozi wa kundi la mataifa tajiri na yale yanayoinukia kiuchumi mkubwa wa viwanda ulimwenguni (G20), umemalizika hivi karibuni mjini New Dehli, India, huku Umoja wa Afrika (AU) ikikubaliwa kuwa mwanachama.

Mkutano huo umemalizika wakati makubaliano juu ya tamko la kulaani kile walichokiita uvamizi wa Russia dhidi ya Ukraine yakipatikana kwa mbinde baada ya mvutano mkali kutokana na mgawanyiko kuhusu vita hivyo.

Siyo nia yangu kujikita kwenye hoja hiyo ambayo imemalizika huku Rais Vladimir Putin wa Russia na mwenzake, Xi Jinping wa China, wakikosekana hapana, bali ni namna gani viongozi wa Afrika wanavyoitazama fursa ya kuwa mjumbe katika kongamano hilo.

Tukianza na kuichambua kauli ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres kuwataka viongozi wa G20 kushughulikia “mkanganyiko” wa hali ya hewa unaoelekea kwenda bila ya udhibiti, utabaini kuwa ni ya muhimu sana kwetu Afrika.

Nasema ni ya muhimu kwa sababu Guterres hakuishia hapo tu, bali alikwenda mbele zaidi kwa kuwasihia kurekebisha kanuni za dunia za kifedha ambazo amezielezea kuwa zimepitwa na wakati.

Na hapa ndipo kwenye hoja yangu, maana inajulikana kwamba, nchi nyingi za Afrika, ikiwemo Tanzania tunakabiliwa na changamoto kubwa ya mabadiliko ya tabianchi yanayotokana na uzalishaji wa taka zinazoharibu mazingira.

Tunapozungumza mabadiliko ya tabianchi maana yake ni kuvurugika kwa mfumo wa majira kwa vipindi vinne vya miezi mitatu mitatu; kipupwe, vuli, kiangazi na masika katika mwaka, kiasi kwamba kalenda ya dunia inaparaganyika kutokana na kuharibiwa na hewa ya sumu.

Kumbuka vinara wa uzalishaji wa taka hizi za hewa yenye sumu duniani ni haya mataifa makubwa yaliyoendelea katika teknolojia ya viwanda vya nyuklia na nchi zote zinazorutubisha uranium.

Hivyo kwa kuwa wapokeaji wa madhira yanayotokana na uharibifu huo ni nchi za Afrika, basi AU isizubae.

Yaani AU watumie fursa hiyo kudai nyongeza ya mgawo wa fedha zitakazotumika kugharamia uchafuzi wa hali ya hewa kwa kiwango sawa na wanavyochafua.

Na kwa kuwa theluthi mbili ya malighafi zinazotumika kwenye viwanda vya hawa G20 inapatikana Afrika, ndiyo utasikia wanashindana kuja kutusaidia ilihali lengo lao kubwa ni kuja kuimarisha mifumo ya kupata zaidi malighafi zitakazotumika kwenye viwanda vyao.

Nihitimishe hoja yangu kwa leo kwa kusema kuwa, sisi wajibu wetu ni kuwakumbusha viongozi wa Afrika kwamba, mataifa haya makubwa yaliyoendelea katika uchumi wa viwanda duniani, lazima yashinikizwe kutoa mafungu ya fedha kuisafisha dunia kama ambavyo wamechangia kwa kiasi kikubwa kuichafua.

• **Mwandishi anapatikana kwa Simu: 0784438546/ Barua-Pepe: mtagaluka@gmail.com**

Habari**Kampuni za bima zaondoa woga**

Na Mwandishi WETU

WAKATI baadhi ya wawekezaji nchini wakihofu kuingiza mitaji sekta ya mafuta na gesi kwa kigezo kuwa inahitaji fedha nyingi, kampuni za bima zimejitosa huko.

Zaidi ya kampuni 20 za bima zimeonyesha njia kwa kutengeneza umoja (konsoti) na kuchanga mtaji unaofikia dola za Marekani milioni sita zitakazotumika kutoa bima kwa watu, mitambo na miradi katika sekta ya mafuta na gesi nchini.

Uamuzi huu una maana kubwa; kwanza, unaonyesha kuwa kuna uwezekano mkubwa wa kampuni na wawekezaji wa ndani kushiriki katika sekta hii muhimu.

Pili, uamuzi huu umeonyesha njia ambayo wafanyabiashara wa ndani wanaweza kuzitumia ili kushiriki katika uendeshaji wa sekta hii muhimu kwa uchumi wa nchi.

Tatu, uamuzi huu unathibitisha kuwa wafanyabiashara wa ndani wana uwezo na wapo tayari kushiriki katika miradi mkubwa yenye manufaa kwa nchi.

Kamishna wa Mamlaka ya Bima Tanzania (TIRA), Dkt. Baghayo Saqware, anasema kuwa ile dhana kwamba Watanania hawawezi kushiriki kwenye shughuli kubwa za uchumi, inazidi kuondoka kupitia uamuzi kama huu wa kampuni za bima.

Ameasema hayo wiki iliyopita alipokutana na waandishi wa habari katika mikutano inayoandaliwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina (TR) ikiwa ni sehemu ya kutambulisha kwa umma shughuli zinazofanywa na taasisi za serikali zinazotoa huduma kibiashara.

“Uamuzi wa kampuni hizi unamaanisha kuwa kama nchi, katika sekta ya bima, tupo tayari na tuna uwezo wa kutoa bima kwa watu, vifaa, miundombinu na miradi itakayohusika katika sekta ya mafuta na gesi nchini,” ameongeza Dkt. Saqware.

Dkt. Saqware anasema kuanzishwa

**Dkt. Baghayo Saqware**

kwa konsoti hiyo ya mafuta na gesi ni moja na mafanikio ya utekelezaji wa majukumu ya TIRA katika kipindi cha miaka michache iliyopita.

Amesema konsoti hiyo, iliyoundwa mwaka jana – 2022 ni moja ya nyenzo muhimu wakati huu nchi inapojitosa katika utekelezaji wa miradi ya mafuta na gesi.

Hivi sasa Tanzania kwa kushirikiana na Uganda, Tanzania inatekeleza mradi wa ujenzi wa bomba la mafuta ghafi (Eacop) kutoka Hoima, Uganda hadi Chongoleani, Tanga. Mradi huo unahusisha uwekezaji mkubwa wa zaidi ya dola za Marekani bilioni nne.

Pia, Tanzania ipo katika hatua za mwisho kuanza utekelezaji wa mradi wa kusindika gesi asilia (LNG) mkoani Lindi.

Konsoti hiyo inaratibiwa na kampuni ya bima mtawanyo ya Tanzania Reinsurance Company Limited (Tan Re) huku kampuni ya Phoenix Tanzania ikiwa ndio kiongozi wa kikundi hicho.

Baadhi ya kampuni zinazounda konsoti hiyo ni pamoja na Phoenix, NIC Insurance, Jubilee, Britam, Heritage, Reliance, UA᠙ Alliance, na Zanzibar Insurance Corporation (ZIC).

Bukoba Raha

... Bukoba kuna senene
... Bukoba kuna maji safi na salama

**Lakini Bukoba kuna G-smart Sauna & Steam Bath
(Bafu la kuoga kwa mvuke).**

**Ukiwa Bukoba ama unaishi, usisahau
kupata huduma G-smart Sauna & Steam Bath.**

**Hakika hautajuta na ona fahari kusimulia
wengine huduma za G-smart Sauna & Steam Bath.**

**Faida za Sauna na Steam Bath ni nyingi,
lakini chache ni zifuatazo:**

- Inaboresha afya ya moyo na mishipa
- Huondoa uchovu wa mwili na misuli
- Kuondoa msongo wa mawazo (stress)
- Kuzuia magojwa ya kukakamaa kwa misuli
- Inaboresha na kuhuisha mfumo wa usingizi
- Kuondoa sumu na kufanya ngozi nyororo zaidi

**Wasiliana na G-smart and Steam Bath
walioko Barabara ya Kashozi na wapigie
simu kwa namba: 0626 265725 / 0767 291 670**

Tangazo

JIKO LAKO : FURSA YAKO

Fursa hii inawakutanisha mawaziri, wabunge, viongozi wa serikali na wajasiriamali wanawake wa Dar es Salaam kwa ajili ya kujenga mnyororo wa kukuza biashara na fursa lukuki.

Hii ni fursa adhimu ambayo kila mwenye kutamani maendeleo binafsi, familia na Tanzania yetu asipange kukosa.

Shughuli: Semina maalum; kutambulisha na kuuza bidhaa; kutoa tuzo kwa wajasiriamali mahiri wa DSM

Mahali: Ubungo Plaza, Ubungo, Dar es Salaam.

Tarehe: 14/10/2023

Muda: Kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi jioni.

**Ewe baba, dada, kaka, mjomba na shangazi, tafadhali
changia maendeleo ya familia na nchi kwa
kuwainua wamama
Karibuni sana kwa fursa lukuki.**

Tiketi

Kawaida Sh. 50,000
(VIP); Sh. 100,000.

Tafadhali wasiliana kwa namba hii ya simu
kwa maelezo zaidi: 0769 014 015

Tunu ya mwanamke uchaguzi 2024

Na Deogratias MUSHI

KATIKA mizania yoyote ile, wanawake ni kundi kubwa lenye nguvu na mchango wake uko bayana; iwe kwenye medani za siasa, maendeleo ya familia na taifa, hivyo haliwezi kupuuzwa.

Ni ukweli usiopingika kuwa idadi yao, wakiwa wapigakura, wanachama wa vyama vya siasa na wazalishaji wanaoendeleza kizazi cha taifa, ni kubwa mno.

Taifa linapoelekea katika uchaguzi wa serikali za mitaa hapo mwakani - 2024, wanawake wanapaswa kutambua na kudai haki za kushiriki katika uchaguzi huo kama wapiga kura na wanaowania nafasi za uongozi.

Mary Nsemwa, mwanaharakati wa usawa wa kijinsia katika jamii hivi karibuni aliendesha semina ya viongozi wa kijinsia kutoka maeneo mbalimbali ya nchi iliyoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) jijini Dar es Salaam.

Katika semina hiyo, Mary alieleza bayana jinsi Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977) inavyobainisha haki za wanawake za kushiriki katika nafasi za uamuzi ikiwa ni pamoja na ushiriki wao katika uchaguzi wakiwa wapiga kura na wagombea nafasi mbalimbali za uongozi.

Msemwa aliwaambia wana semina kuwa wanawake wanapaswa kudai ushiriki wao katika uongozi wa taifa, ikiwa ni pamoja na kushiriki katika uchaguzi ujao kama wapiga kura, watueliwa kuwania nafasi mbalimbali na hatimaye kutangazwa washindi ili kuwakilisha wananchi katika vikao vya uamuzi.

Mwanaharakati huyu anashauri kuwa vyama vya siasa, tangu wanachama, uongozi na mashabiki wa vyama hivyo wakubali wanawake kuwania nafasi mbalimbali za uongozi na hiyo inaweza kuwa njia pekee ya kuingia kwenye kinyang'anyiro cha uchaguzi.

Mkufunzi kutoka TGNP, Anna Sangai,



Lilian Liundi- Mkurugenzi TGNP

anasema serikali iliyoko madarakani ina wajibu mkubwa wa kuhakikisha kuwa uwanja wa ushindani wa kisiasa ni huru, wenye usawa na salama kwa makundi yote hususan wanawake.

Sangai anatoa mwito kwa wanawake kutambua kwamba kura zao ni turufu ya ushindi kwa vyama vyao vya siasa na wagombea, hivyo uchaguzi wa mwaka kesho wa serikali za mitaa ukifuata misingi hiyo, utakuwa wa kihistoria kwenye harakati za ukombozi wa wanawake kimapinduzi hapa nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Liundi anaasa kuwa wakati Tanzania inajiandaa kuingia kwenye uchaguzi wa mwaka 2024, wanawake, wanamtandao, watetezi wa haki za wanawake, wanapaswa kutafakari harakati za kumpa fursa mwanamke zilipotoka, mafanikio yaliyopatikana, changamoto, na mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo kwa sasa.

Lilian anasema kuwa kipindi hiki ni kipindi muhimu kitakachowezesha kutafakari kuhusu maendeleo ya wanawake kwa ujumla wakati huohuo kikiwa ni kipindi cha kubainisha mbinu mbadala za kuendeleza mapambano ya kuongeza wanawake wenye sifa za uongozi katika kisiasa.

Utalii**Kenya wamlilia mtangaza utalii**

Na Mwandishi WETU,
Nairobi

ZAIDI ya miaka 41 iliopita, Kenya ilikuwa tayari imepiga hatua kubwa katika kutangaza utalii wake.

Maeneo mengi duniani walielewa kwamba unapozungumziwa utalii wa kutazama wanyama anuai wanaopatikana Afrika, basi ilikuwa nchi sahihi ya kuwaona simba, faru, nyati, viboko, nyumbu na hata ndege wa aina tofauti.

Kufahamika kwa Kenya kwamba ni kitovu cha utalii, kulikomazwa zaidi na mwimbaji wa Uingereza, Roger Whittaker ambaye aliitembelea nchi hiyo ya Afrika Mashariki na kuipenda zaidi.

Kuipenda Kenya aliamua kuenzi na kuutangaza utalii wake kwa dunia nzima kupitia wimbo uliokuja kuwa maarufu zaidi ukiitwa; *My land is Kenya* (Nchi yangu ni Kenya).


Wimbo huo ukiwa na mahadhi ya “country,” ingawa baadaye watu wengi wakapenda kuupa vionjo vipya vya “wimbo wa safari.”

Tangu mwaka 1982, wimbo huo umekuwa ukitumika zaidi kuitangaza Kenya na utalii wake maeneo mengi duniani, na hakika umefanya kazi kubwa ya kuitambulisha nchi hiyo na urithi wake kwa dunia nzima.

Hata hivyo, pamoja na kwamba wimbo huo utadumu kwa miaka mingi, mtunzi wake, Whittaker wiki iliopita, aliaga dunia akiwa na miaka 87.

Taarifa zilizofika kwa Pambazuko zinaeleza kwamba mwanamuziki huyo alifariki dunia Jumatato – September 13 akiwa anapata matibabu katika hospitali moja kusini mwa Jiji la Paris, Ufaransa.

“Maisha yake, usanii na urithi wake umekuwa wa maana sana kwa wengi duniani kote. Tunashukuru kwamba zawadi ya muziki wake inabaki kwetu,” rafiki yake Jesse Wagoner alisema wakati



Roger Whittaker

akitangaza kifo hicho.

Whittaker ambaye wazazi wake walikuwa Waingereza alizaliwa katika mji mkuu wa Kenya, Nairobi na kupata makuzi yake huko, kabla ya kurejea kwao na baadaye kuwa “mgeni” wa mara kwa mara nchini humo.

Moja ya mashairi ya kuvutia ndani ya wimbo huo ni haya;

My land is Kenya, so warm and wild and free,

You'll always stay with me here in my heart

My land is Kenya, right from your highlands to the sea

You'll always stay with me here in my heart, here in my heart.

Kufuatia kifo hicho, Wakenya wenye umri kuanzia miaka 40 na kuendelea wanakumbuka sauti na vionjo vya wimbo huo maarufu na kwamba mtunzi huyo ataendelea kukumbukwa kwa muda mrefu.

Viongozi mbalimbali wa Kenya wamemlilia mwanamuziki huyo na kumpa sifa kubwa za namna wimbo wake umeupaisha utalii wa nchi hiyo.

“Miaka mingi, zaidi ya 40, Kenya imetambulishwa duniani kote na muziki wa Whittaker na umekuwa

Ni wakati wa e-GA kung'ata

Na Mwandishi WETU,

KATIKA toleo namba 0046 la gazeti hili, safu mpya ya Jicho la Tai iliripoti kuwepo kwa taarifa zisisokuwa sahihi kwenye uendeshaji wa tovuti ya Ofisi Namba Moja nchini – Ikulu.

Kwamba katika tovuti hiyo ilikuwa hajichapisha kwa usahihi mabadiliko ya Baraza la Mawaziri yaliyokuwa yamefanywa na Rais siku kadhaa nyuma. Kulikuwa na mawaziri waliobadilishwa nafasi, lakini wakatambuliwa kwa nafasi pia za awali na pia alikuwepo waziri ambaye alishaondolewa kwenye nafasi ya uwaziri, lakini tovuti iliendelea kumtambulisha kuwa waziri.

Hata hivyo, baada ya kutolewa kwa umma taarifa hizo, Ikulu ilichukua hatua haraka na kurekebisha – kwa usahihi, maudhui ya tovuti hiyo.

Lakini kama unadhani kuwa udhaifu wa kuhuisia tovuti katika ofisi za umma unaishia hapo, basi utakuwa unafanya kosa kubwa.

Tovuti nyingi za taasisi za serikali zina taarifa zilizopitwa na wakati huku zikikosa taarifa ambazo zinapaswa kuwepo.

Inasikitisha kuwa hali hii inajitokea katika mazingira ambayo serikali imewekeza kwa kiasi kikubwa sana kuimarisha matumizi ya tehamu ili kurahisisha utendaji kama nyenzo ya kusukuma gurudumu la maendeleo kwa kasi kubwa.

Kwa kuziona juhudi hizo za serikali, wadau kutoka sekta binafsi ya washirika wengine waliamua kuchangia kwani waliamini kuwa kupitia matumizi ya tehamu, serikali itajikomboa haraka katika harakati zake za kuboresha utendaji na kuimarisha mawasiliano kwa kuimarisha mawasiliano.

Lakini inasikitisha kuwa kwa kiasi kikubwa juhudi hizi zinafishwa.

Inasikitisha kuwa licha ya juhudi zote ambazo serikali inazichukua kuimarisha matumizi ya tehamu katika ofisi zake, mpaka leo, siyo tu kuwa tuna tovuti ambazo zinatoa taarifa potofu, bali mifumo muhimu katika uendeshaji wa



Benedict Ndomba - Mkurugenzi Mkuu wa e-GA

uchumi wa nchi, baina ya taasisi za umma, haisomani.

Turejee nyuma kidogo

Septemba mwaka 2016, rais wa serikali ya awamu ya tano, John Magufuli, alifanya ziara ya kushitukiza katika Bandari ya Dar es Salaam.

Kati ya mambo aliyoyashuhudia katika ziara hiyo ni kuwepo kwa mitambo ya kuchunguza mizigo inayoingia kupitia bandari hiyo (skana) ambayo mifumo yake ya mawasiliano haikuunganishwa na mifumo ya mkusanya kodi mkuu nchini - Mamlaka ya Mapato (TRA).

Siyo hilo tu, ofisa wa TRA ambaye alikuwa anahusika na ukaguzi wa mizigo ambayo inapita katika skana ili kujua kodi halisi inayopasa kutozwa kwenye mizigo hiyo, alikuwa amewekwa kwenye chumba ambacho hakina hata madirisha.

Kwa maana hiyo alikuwa hata hawezi kuona moja kwa moja makasha au mizigo inayopitishwa kwenye skana.

Huyu alikuwa anatategemea mtu wa skana akishamaliza kazi zake ndipo amletee taarifa na takwimu kuhusu mizigo iliyochunguzwa!

Rais Magufuli alipouliza kwa nini hali iko hivyo alipewa maelezo marefu ambayo kimsingi yalikuwa yanamwambia kuwa mifumo kati ya Mamlaka ya Uendeshaji wa Bandari (TPA) na TRA ilikuwa haisomani.

Hili lilikuwa ni jambo la kushitua sana kwa sababu lilimaanisha kuwa

Makala**Ni wakati wa e-GA kung'ata***Inatoka Uk. 15*

mizigo ambayo ilikuwa ndio inapaswa kuingiza mapato ya kodi, ilikuwa inapita bandarini bila ya mkusanya kodi kujua uhalisia wake.

Labda hii ni moja ya sababu zilizofanya serikali ya awamu ya tano kuanzisha Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) ambayo nayo ikaanzisha mtandao wa mawasiliano serikalini (GovNet) ambao ni salama, rahisi na wenye kuaminika kwa ajili ya kurahisisha mawasiliano ndani ya serikali.

Tovuti ya mamlaka hiyo inaeleza kuwa kutokana na jitihada hizo, wizara, idara na wakala 72, mamlaka za serikali za mitaa 77 katika mikoa 20 ya Tanzania Bara na taasisi za umma 18 zilizopo Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma zimeunganishwa kwenye mtandao huo.

Nyingine ni hospitali za mikoa, ofisi za sekretarieti za mikoa, halmashauri za wilaya na manispaa au jiji.

Kwa kutambua umuhimu wa mtandao huo, e-GA ilianzisha Kituo cha Uendeshaji Mtandao (Network Operating Centre-NOC) kinachofanya kazi wakati wote kwa lengo la kusimamia na kushughulikia hitilafu na matatizo mtandao huo.

Lakini, licha ya hayo yote tumeshuhudia mara kadhaa wafanyabishara wakikwama kukamilisha malipo ya ushuru na kodi mbalimbali kupitia TRA kwa sababu eti mtandao uko chini!

Lakini, hii ni sehemu tu ya matatizo makubwa kuhusu matumizi ya tehamu katika taasisi za umma.

Mamlaka na nyenzo hizi zilianzishwa ili kuwezesha mifumo ya serikali kusomana. Moja kati ya mifumo nyeti tuliyotarajia itashughulikiwa kwa haraka ni kati ya Bandari na TRA.

Siku chache baada ya ziara hiyo ya kushitukiza ya Rais Magufuli bandarini, zikatolewa taarifa kuwa mradi wa kuweka mashine mpya za kisasa za kukagua mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam ambazo zina uwezo wa kusoma na kupeleka taarifa na picha za mizigo mubashara kwenye mifumo ya TPA na

**Dkt. Mussa Kissaka - Mwenyekiti wa Bodi ya e-GA**

TRA ulikuwa umekamilika.

Lakini, hatujui ni nini kimetokea kwa mfumo huo mpya kwani hivi karibuni Rais Samia Suluhu Hassan naye amesikika akilalamika hadharani kuwa mifumo ya TPA na TRA haisomani.

Akatoa maagizo kuwa wataalamu kutoka nje ya nchi ambao walikuwa wanafanya kazi ya kuimarisha mifumo ya mawasiliano TRA wasiondoke nchini hadi watakapohakikisha mifumo ya mawasiliano ya TRA inasomana na ile ya TPA.

Ni mifumo ileile ambayo mwaka 2016 Rais Magufuli alibaini kuwa haisomani. Serikali ikaanzisha mamlaka mahsusi kushughulikia suala hilo siyo kwa Bandari na TRA tu, bali serikali nzima.

Leo hii, miaka zaidi ya minne baada ya mamlaka hiyo kuanzishwa mwaka 2019, bado mifumo ya Bandari na TRA haisomani kama ambavyo Rais Samia amethibitisha katika kauli yake!

e-GA inasema kwenye tovuti yake kuwa dhima yake kubwa ni kuratibu, kusimamia na kukua jitihada za serikali mtandao pamoja na kuhimiza utekelezaji wa sera, sheria, kanuni, viwango na miongozo ya serikali mtandao kwa taasisi za umma.

Ilikuwa na dhima hiyo tangu ilipoanzishwa na serikali ya awamu iliyopita. Leo hii tuko awamu ya sita bado mkuu wa nchi analalamika hadharani kuwa mifumo ya TPA na TRA haisomani. Ni wakati e-GA wakatueleza

Ni wakati wa e-GA kung'ata

Inatoka Uk. 16

kwa nini hali kama hiyo inatokea na wao wapo?

Tovuti hali mbaya

Kwa upande wa tovuti za taasisi za umma hali ni mbaya zaidi licha ya jitihada za serikali yenyewe na taasisi binafsi kusaidea kuboresha utendaji.

Miaka kadhaa iliyopita, NGO moja ya Wamarekani, Pact Tanzania, ilitoa mafunzo kwa maofisa habari na mawasiliano wa halmashauri zote nchini jinsi ya kuanzisha na kuendesha tovuti.

Lengo lilikuwa ni kurahisisha mawasiliano ndani ya halmashauri na kuhakikisha taarifa zinawafikia wananchi kwa haraka.

Kama sehemu ya mafunzo hayo halmashauri zote zilisaidiwa kuanzisha tovuti zake.

Hata hivyo, leo hii tovuti za halmashauri nyingi nchini ni mfu. Zipo baadhi zinajikongoja, lakini ni kama zinapumulia mashine maana uhuishaji wa taarifa unachukua muda mrefu sana.

Zile ambazo bado zipo hai nazo zinaendesha kwa mashaka kwa sababu licha ya kuwepo kwa taarifa nyingi katika halmashauri, lakini ni taarifa chache tu ndizo utazikuta katika tovuti hizo na uhusishaji wa taarifa huchukua muda mrefu.

Kuna baadhi ya wizara nazo zina tatizo sugu katika uendeshaji wa tovuti zake. Taarifa huchelewa sana kuwekwa na taarifa zinazowekwa ni chache sana ukilinganisha na taarifa ambazo zinaihusu wizara husika.

Idara ya Habari - Maelezo ndio ilipaswa kuwa mlezi wa vitengo hivi vya habari katika taasisi za umma, lakini siku hizi nayo imejikita katika kuchakata na kusambaza maudhui yake mitandaoni.

Sijui kama inapata muda wa kuhakikisha kuwa taasisi za serikali zinaendesha tovuti zao ipasavyo.

Vitambulisho shida nyingine

Shida hizi za tehamu zipo pia kwenye mifumo ya utambuzi.

Katika nchi zilizoendelea, kila



Mifumo ya utendaji serikalini inapaswa kusomana.

mwananchi anakuwa na namba moja tu ya utambulisho ambayo itamtambulisha katika huduma yoyote anayoihitaji.

Uingereza kwa mfano, wana namba ya utambuzi (NI), ambayo kila mtu aliyefikisha umri wa miaka 16 anapatiwa.

Namba hiyo inamtambulisha mtu kama mlipakodi na inatumika anapohitaji huduma yoyote iwe kutaka leseni ya udereva, kuomba kazi, kwenye matibabu na huduma nyingine zote.

Lakini hapa kwetu mambo ni shaghalabaghala. Mtu mmoja ana namba za utambuzi lukuki; Ukienda kukata leseni ya biashara TRA watakupa TIN namba, ukienda kukata leseni ya udereva utapatiwa namba nyingine ya leseni ya udereva, ukijiunga na mfuko wowote wa hifadhi ya jamii huko nako utapatiwa namba nyingine ya utambulisho.

Ilipokuja NIDA nayo ikatoa namba za kuwatambua Watanzania na wageni waliosajiliwa kupitia mfumo huo.

Kwa hiyo utakuta mtu mmoja anatambuliwa kwa namba nyingi.

Mbaya zaidi, mifumo hii yote inayotoa namba za utambulisho, nayo haisomani!

Kwa muda sasa kumekuwa na mapendekezo kuwa Mtanzania atambuliwe kwa namba moja tu na taarifa zake zipatikane katika mifumo yote ambayo atahitaji huduma.

Lakini licha ya uwepo wa e-GA, utekelezaji wa hilo nao umekuwa mgumu sana, nah ii inatokana na mamlaka hiyo kutokuwa wafuatiliaji na wakali kuhakikisha Tanзания inakuwemo kwenye bwawa la mawasiliano ya kisasa na rahisi zaidi.

Riwaya

Tetemeko la ndumba - 3

Mtunzi: Innocent N. ZAGALLO

Akapenya ndani ya pori hilo, Aakitembea taratibu huku akijitahidi kuiepuka miba na kujihadhari na nyoka waliosemekana kulitawala eneo hilo. Alikuwa makini wakati akilivaa pori hilo, akiangaza macho huku na kule na kwenye mti huu na ule hadi alipokomea chini ya mti aliouhitaji.

Akautazama mti huo huku kwa mbali akitetemeka. Hakuwa akitetemeka kwa hofu, bali alitetemeka kutokana na baridi kali iliyopenya maungoni mwake. Akafungua ule mfuko wake mweusi na kuchomoa kisu. Akausogelea mti huo na kuanza kuuparua magamba taratibu na kwa umakini wa hali ya juu.

Magamba hayo alikuwa akiyaweza ndani ya mfuko huo. Alipotosheka na idadi ya magamba aliyopata, alianza safari ya kurejea nyumbani, moyoni akiwa amesuzuka kwa mafanikio ya safari yake.

Alipofika nyumbani hakuwa na haraka ya kumtaarifu chochote mkewe. Alitulia hadi baada ya mlo wa usiku ndipo alipomwita na kumwambia, “Kesho n'taondoka.”

“Sijakuelewa, baba Shaka,” mkewe alisema huku akiondoa vyombo vilivyotumika kwa maakuli.

“Kesho n'taondoka!” Mzee Songoro aliirudia kauli yake, safari hii kwa msisitizo. “Nakwenda Dar kumkomboa mwanangu.”

“We baba Shaka, utamkomboaje mwan'etu?” Mama Shaka aliuliza huku akiacha kufanya kila alihokuwa akikifanya. Akasimama wima na kumtazama mumewe kwa mshangao, mikono kaikita kiunoni

“Hayo nitayajulia hukohuko,” Mzee Songoro alisema. “Lakini kwenda ni lazima. Nina hakika Shaka hataendelea kusota gereza, labda mimi nisiwe Songoro niliyezaliwa Tongwe na kukulia



Uganga

Kasingirima Ujiji kabla ya kuja kujenga huku Mwangi.”

Naam, Mzee Songoro hakuwa na mzaha kuhusu suala hilo. Alidhamiria kumtoa mwanaye kifungoni, iwe, isiwe.

Asubuhi ya siku iliyofuata alikwenda Stesheni na kuonana na mtu mmoja, mfanyakazi wa Shirika la Reli ambaye alimpatia tikiti ya Daraja la Tatu ya kumtoa Kigoma hadi Dar es Salaam.

Kisha alirudi nyumbani na kuanza kujiandaa rasmi kwa safari hiyo ya dharura. Alikwenda kwenye duka la jirani ambako alinunua chupa ya maji yenye ujazo wa nusu nusu lita, akaweza akayanywa maji kidogo mbele ya muuza duka kisha akaondoka na mbele kidogo akayamwaga maji yaliyosalia.

Kwa kujidai akaenda nyumbani ambako alitwaa yale magamba aliyoyatoa porini jana yake na kuanza kuyaponda.

Zoezi la kuyaponda magamba hayo lilidumu kwa takriban nusu saa hadi yakalainika na kupatikana unga ambao ndio ulikuwa muhimu kwake. Akautwaa unga ule na kuumimina kidogo ndani ya chupa ile ya maji. Unga mwingine aliuweka ndani ya kijichupa kidogo. Kisha alitwaa mzizi, akauzungushia karatasi na kuuweka kando ya ile chupa ya maji.

Itaendelea toleo lijalo...

Watoto

BKF chachu ya vipaji, elimu

Na

Nestory
NESTORY

MARA nyingi vipaji vinavyooneana kwa watu wazima, vina mzizi wake tangu utotoni.

Kwamba ikiwa dalili za umahiri wa kucheza kuimba, kupenda kusoma vitabu, kufurahia hesabu na ubunifu wowote, huchomoza katika umri mdogo wa mtoto.

Wataalamu wa makuzi ya binadamu wanaeleza kuwa umri wa vipaji kugundulika na kuanza kuonekana kwa binadamu, ni miezi tisa ya mwanzo ya mtoto.

Ikiwa mtoto anabainika kuwa msikivu, mtulivu, asiyependa kelele, basi huyo huenda akawa na kipaji kinachohitaji zaidi umakini katika shughuli zake atakapokua.

Ikiwa mtoto anapenda kucheza, kufurahi, kujitikisa kila anaposikia sauti za muziki, basi huyo atajenga mazoea ya kupenda shughuli zenye "hekaheka."

Hata hivyo, siyo kila mtoto hupitia dalili, wapo wasioonyesha chochote hadi wanapokuwa wakubwa, na wengine mazoea ya wanaoishi nao, huweza kuwapa njia ya kupenda kipaji fulani.

Kimsingi, vipaji hulelewa na kukuzwa na hapo ndipo kunapohitajika waelekezi na wenye kupenda watoto kuwa nao sambamba.

Ni kutokana na utambuzi huo,

mwalimu
Dorice
Lyimo wa
Shule ya
Awali na
Msingi Moga
iliyoko Bunju,
Dar es Salaam
na rafiki yake,
Aileen Mushi,
waliaamua



kutumia ujuzi wao kusaidia watoto kukuza vipaji wanapokuwa nje ya madarasa ya shule.

Wataalamu hao wa malezi, wameanzisha tamasha la watoto wa shule wanapokuwa likizo, ambalo lina lenga kukutanika watoto kutoka shule mbalimbali ili kuwapa elimu wasiyoipata darasani, kukuza na hata kutambua zaidi vipaji vyao.

Tamasha hilo linaloitwa; Bunju Kids Festival (BKF) lililofanyika Bunju, linatarajiwa kuwa endelevu kwa kila wakati watoto wanapokuwa likizo.

Katika kutekeleza ndoto za wataalamu hao wa malezi ya watoto, walifanya tamasha la kwanza Septemba 13, 2023 na kuvutia watoto zaidi ya 50, ambao walijifunza vitu vingi ikiwamo namna ya kuishi na wenzao wanaokutana kwa mara ya kwanza.

Pia watoto walijifunza namna ya kutengeneza mifuko ya karatasi na bidhaa mbalimbali, kucheza, kula na kunywa.

Tamasha lingine limepangwa kufanyika Desemba mwaka huu wakati watoto watakuwa nyumbani kwa mapunziko ya mwisho wa mwaka na sikukuu za Krismas na Mwaka Mpya.

KINYWAJI SI NDIO HIKI!



Serikali ya China imepania kutangaza zaidi vivutio vya utalii na fursa mbalimbali zinazopatikana Tanzania ili kuvutia raia wake. Hiyo ni ahadi ya Balozi wa China nchini Tanzania Chen Mingjian kupitia njia mbalimbali. Pichani ni baadhi ya watalii kutoka China walipowasili Dar es Salaam kuanza utalii. (Picha kutoka mtandao wa X wa Balozi Chen).

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.

